# LEARNING BY EAR 2012

# “Bado ningali mwanadamu – Riwaya inayoangazia matatizo wanayopata wauguaji wa maradhi ya akili barani Afrika”

## EPISODE 4: “Maadili mema na maovu”

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Pendo Paul**

**PROOFREADER: Pendo Paul**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: KWA MALEMBA KUMEZUNGUKWA NA MAJIRANI**

- **Mtu (mume, 45)**
- **Sauti mchanganyiko (3 hadi 4 , wake + waume, 30 +)**
- **Msimulizi**

**SCENE TWO: KAPAKA AWAZA KUJINYONGA**

- **Kapaka (mume, 25)**
- **Cheupe (mke, 25)**
- **mchungaji (mume, 40)**
- **MSIMULIZI**

## SCENE THREE: VALERIE AKIWA NJIANI

- **Valerie (mke, 19)**
- **MLINZI (mume, 30)**
- **MSIMULIZI**

## SCENE FOUR: MALEMBA ARUDI NYUMBANI BAADA YA KUOKOTA KUNI

- **Malemba (mke, 35)**
- **Chumba (mume,16)**

**UTANGULIZI:**

Salam tele na karibu tena katika kipindi cha **Noa bongo, Jenga maisha yako**. Hadithi ni ileile ya, **“Bado ningali mwanadamu”,** na inahusu suala nyeti la maradhi ya akili barani Afrika. Kipindi kilichopita, Malemba alimpeleka kijana wake Chumba kwa Mizanja, mtabibu wa kienyeji, baada ya kukataliwa kupewa huduma katika hospitali moja hapo mtaani. Na Valerie naye alikwenda kumtembelea daktari wa pekee nchini aliye na taaluma ya akili, Dkt. Mahiro, aliyemshauri kumtembelea kila wakati. Sasa ni yapi yalioivishwa katika kipindi hiki cha leo? Hebu tushuhudie. Kipindi hiki kinaitwa **“Maadili mema na maovu”.** Tunaosha uso kijijni ambapo majirani walikuwa wameizunguka nyumba ya Malemba.

**SCENE ONE: NYUMBA YA MALEMBA IMEZUNGUKWA NA MAJIRANI**

1. **ATMO:** **VILLAGE AMBIENCE AT DAWN**

2. **MAN:** **(shouting)** Malemba! Wewe mchawi toka nje! Tumechoshwa na uchawi wako. Leo ni leo!

3. **MIXED VOICES: SCREAMING AND YELLING “MCHAWI ACHOMWE”**

4. **MTU:** Malemba, usipotoka, kwa hakika hiki kijumba chako tutakitia moto! Husikii? Hatutaki kuishi na wachawi tena! Siku yako ni leo...

5. **SAUTI MCHANGANYIKO: SHOUTING “Choma mchawi”**

6. **MTU:** Leo utaona hatima yako. Ikiwa wataka salama yako toka! Sawa maadamu anafikiria tunafanya mzaha, mwenye kiberiti anipe.

7. **SFX:** **MATCHBOX BEING LIT UP**

8. **MTU:** Malemba, wewe na uovu wako nyote mteketee ndani ya moto huu! Jamii haitaki watu kama wewe, hata kijana wako mwenyewe Chumba, umemtoa kafara na kuleta laana katika kijiji chetu. Mvua imekatika, mifugo yetu inakufa na watu wetu kupukutika kwa mauti. Hatukuui kwa kuwa twakuchukia, la, ni kwa sababu tunataka kutakasa kijiji chetu!

9. **SFX:** **GRASS CATCHES FIRE AND STARTS TO BURN**

10. **MTU:** Haya kila mtu kwao kwao, au sivyo mapepo wakitoka kwenye nyumba ile watawaingia nyinyi...mbio kila mtu!

11. **SFX:** **PEOPLE SHOUTING AND YELLING AS THEY RUN AWAY, FADE IN BACKGROUND.**

12. **MSIMULIZI:** Maskini kijumba cha Malemba hakikihumili biwi la moto ule! Kwa sababu ya kipupwe cha alfajiri ile, moto ulienea kwa kasi. Na baada ya dakika za kutema mate yasikauke kijumba cha Malemba kilikuwa kimelala kifudifudi. Kweli ni haki kwa majirani kutekeleza uhaini kama ule? Kisa na sababu wana shauku kuwa Malemba ni mchawi? Kwani kuuguwa wendawazimu sharti mtu awe amerogwa? Labda swali jengine unalojiuliza ni: ni yapi yaliowafika Chumba na Malemba? Huu ndio mwisho wao? Usitaharuki, jibu liko njiani laja. Kwa sasa, hebu tufungue ukurasa wa Kapaka. Alipopoteza kazi yake, pia alipoteza hamu ya kila kitu. Alikumbwa na yale maradhi wataalamu huyaita “clinical depression” hali inayokupa kujihisi huna thamani tena. Lakini Kapaka na mkewe Cheupe hawafahamu haya. Kwa hivyo, mkewe Cheupe anamleta nyumbani mtu aliyefikiria anaweza kumsaidia mumewe.

## <u>SCENE TWO: KAPAKA ANAWAZA KUJINYONGA</u>

13. **KAPAKA:** Sina maana, sina tumaini, sina msaada wowote. Nimesalia kuwa duni sina thamani. Fukara kama mimi nawezaje kuwa mume wa mtu, sifai kuwa hata mshirika licha ya rafiki, ujirani wa kuomba utatakiwa na nani. Karibuni nitaitwa baba... itakuaje? Haiwezekani! Maisha gani haya ya kuwa unaishi na huwezi kuwa unavyotaka mwenyewe, huwezi hata kupata unachotamani

kuwa nacho?

14. **SFX:** **PAPER BEING TORN FROM BOOK**

15. **KAPAKA:** Nimefikwa na yakutosha katika aibu hii. Siwezi kusubiri mtoto wangu azaliwe na anione jinsi nilivyo hohehahe. Nimeshindwa kumhudumia yuko tumboni sembuse akizaliwa... mimi sina thamani kwa familia yangu, ukoo na hata watu wangu. Sawa, wacha niandike barua hii haraka kabla Cheupe arudi kutoka kanisani.

16. **SFX:** **PEN SCRIBBLING ON PAPER**

17. **KAPAKA:** **(takes a deep breath / reads as he writes)** Kwa muhibu wangu Cheupe, mpendwa mke wangu. Nisamehe kwa machungu nitakayokupa, nimeamua kukatisha maisha yangu kwa sababu nilimaliza kuishi zamani. Tafadhali usilie. Mlee vizuri mtoto wetu. Pole sana.
**(stops writing, sudden anger)** Naichukia hii dunia na kila kitu! Wakati wa kuchukua hatua ni sasa! Nataka kulipa makosa yangu. Arrrgh!!
**(bangs his head on the table several times)**

18. **SFX:** **HEAD BANGING ON WOOD SEVERAL TIMES**

19. **KAPAKA:** Ah, kichwa kinaniuma. Siwezi tena kustahimili. Cheupe haelewi ninavyohisi. Hakuna anaye

elewa, na hakuna anayejali. Dunia katili. **(starts to cry)** Mama na baba, karibuni nitaungana nanyi mapumzikoni: futi sita chini ya dongo la tifu. Labda huko nitapumzikoa na haya madhila na mateso haya.

20. **SFX:** **DOOR BEING KNOCKED**

21. **KAPAKA:** **(faintly)** Niacheni. Nataka kufa kwa amani. Tafadhali nenda. Nataka nife peke yangu.

22. **CHEUPE:** **(from outside)** Kapaka! Ni mimi mpenzi. nimerudi, na nimekuja na mtu kutoka kanisani. Fungua mlango sioni funguo tunapoziweka, funguo sizioni.

23. **KAPAKA:** Cheupe, Samahani. Kila kitu nimekuandikia. Kila kitu kitakuwa sawa. Utaona waraka wangu.

24. **CHEUPE:** Mchungaji, unaona ninachomaanisha? Nina kuambia: Kapaka siye yule unayemjua kawaida yake. Anamaanisha nini kuwa kila kitu kimeandikwa katika waraka?

25. **MCHUNGAJI:** Haraka! Fungua mlango, nahofia labda anataka kujidhuru!

26. **CHEUPE:** Oh Mungu wangu! Hapana. Haiwezekani….funguo zangu ziko wapi…

27. **SFX:** **SOMEONE FUMBLING WITH A HANDBAG**

28. **MCHUNGAJI:** Hatuna muda… tafadhali, itanibidi nivunje huu mlango.

29. **SFX:** **DOOR BEING KICKED OPEN**

30. **SFX:** **TWO PERSONS STORMING IN**

31. **MCHUNGAJI:** Uko wapi, Kapaka? Uko wapi?

32. **CHEUPE:** **(breathing heavily)** Ame…Ame…. ameketi pale chini, kando ya kabati.

33. **MCHUNGAJI:** Kapaka, Tafadhali usinywe hiyo. Niko hapa kukuombea. Mke wako amenieleza yote.

34. **CHEUPE:** **(going into labour)** Oh...fyu! ni mtoto! Anakuja... nasikia uchungu... Aaah….

35. **MCHUNGAJI:** **(confused)** Ati!? Saa hii? Sawa ... tutaanzia wapi?

36. **CHEUPE:** **(screaming)** Aaaah…Kapakaaaa…amka! Mtoto wetu anakuhitaji.

37. **MCHUNGAJI:** **(panicking voice)** Ndio! Kapaka, mke wako anakuhitaji, mtoto wako anahitaji baba. Usiwadhulumu furaha hiyo.

38. **KAPAKA:** **(sudden change of mood)** Cheupe mkewangu! Uko sawa? Oh Mungu wangu. Kwani wakati umefika! Kwani nimekuwa wapi? Sawa, mchungaji, tumharakishe hospitali haraka. Umekuja na gari sio?

39. **MCHUNGAJI:** Vyema, sawa, lakini ungelipata kuoga kwanza? Badilisha nguo, una harufu mbaya ya mtu alioyekosa kuoga kwa juma zima...

40. **CHEUPE:** **(more screams)** Aaaah... fuuuu... **(short breathing)** nasikia mtoto amesimama…harakisheni…

41. **PASTOR:** Sawa, twende, sote!

42. **MSIMULIZI:** Kitoto kichanga cha Kapaka kimemuokoa babake kutoka kwenye tangalachi. Waathirika wengi kama Kapaka hawapati fursa hii. Maradhi haya ya “sononi” hugeuza mtazamo wa jinsi mtu anavyojiona , maisha yake, na wale walio karibu yake. Lakini Waafrika wengi hawajui dalili hizi, sababu au jinsi ya kutibu maradhi haya. Wakati watatu hao wakielekea hospitali, wanafunzi katika chuo cha uuguzi wako katika mapumziko. Lakini Valeri hayuko miongoni mwao. Pia hajarudi kumuona Dkt. Mahiro, na hali yake imezidi kuwa mbaya. Ametoroka chuoni, na hivi sasa analala kwenye majalala ya mjini, anazungukazunguka na kuzungumza na kila anayepishana nae njiani. Anabwabwaja kwa sababu maneno yake hayana maana yeyote.

**SCENE THREE: VALERIE AKIWA NJIANI**

43. **ATMO:** **BUSY STREET AMBIENCE**

44. **VALERIE:** **(laughing)** Mimi ni daktari… na wewe ni mgonjwa! **(laughs uncontrollably)** Hei! **(calls to stranger)** Hei wewe, ndio, wewe ndiye mgonjwa! Njoo hapa… njoo kwa daktari. Hahahaha. Kuna nini? **(talking to self)** usiniongeleshe! Usinikaribie!

45. **MSIMULIZI:** Kama maradhi mengine, maradhi ya akili yasipotibiwa kwa wakati unaofaa huibuka na kuleta shida nyengine kubwa zaidi. Valerie, msichana mwenye ukakamavu wa kuwa muuguzi mahiri, sasa anazungukazunguka mitaani, amevaa matambara sababu ya kuzidi kutengwa na watu na matusi mengi ambayo anatusiwa na watu wasiojua hata maradhi yake yanasababishwa na nini - kama yule mlinzi aliyepo pale Valerie alipoketi.

46. **MLINZI:** Wewe msichana kichaa! Toka hapa karibu na mlango– unanifukuzia wanunuzi. Sogea huko, potea!

47. **VALERIE:** **(laughing)**

48. **MLINZI:** Unanichekea? Unafikiri ninacheka na wenda wazimu kama wewe? Ninakwambia toka hapa, au nikufurumushe!

**Silence**

49. **VALERIE:** **(more laughing)** Wewe ni mgonjwa! Mimi ni daktari!

50. **MLINZI:** Sasa, nimechoshwa na huo wazimu wako, ngoja nikuonyeshe cha mtema kuni!

51. **SFX:** **SOMEONE BEING ROUGHED UP**

52. **VALERIE:** **(complaining)** Hmm... nitakuuma!

53. **MLINZI:** **(screams in pain)** Arrrrgh ...wewe wazimu mshenzi!

54. **SFX:** **HARD SLAP ON FACE**

55. **VALERIE:** **(begins to weep)**

56. **MLINZI:** Usikaribie hapa la sivyo nitagonga hicho kichwa chako mpaka urudi akili timamu!

57. **MSIMULIZI:** La kusikitisha ni kuwa, hayo ndiyo mazoea mabaya tuliyo nayo wengi wetu inapohusisha kuishi na watu wenye maradhi ya akili. Wengi wanafikiri wendawazimu hawafikirii, hawahisi… kwa ufupi hawawahesabu kama binadamu. Matukio ni mengi kuhusu dhulma za watu hawa, kimwili na hata kingono. Valerie tayari amepitia dhulma. Je itakua mara hiyo pekee? Tunapoondoka njiani, tuelekee makazi ya Malemba ambayo yamekuwa majivu kwa

sasa. Lakini majaliwa ndiyo yaliyomtoa Malemba kwenda kuchukua kuni na kumnusuru kuchomwa moto. Tuangalie ni yapi yaliyojiri aliporudi nyumbani.

**SCENE FOUR: MALEMBA ARUDI BAADA YA KUOKOTA KUNI**

58. **SFX:** **EMBERS STILL BURNING**

59. **MALEMBA:** **(singing a song, suddenly stopping)** La!!! Chumbaaaaa! Mwanangu!!!

60. **SFX:** **BUNDLE OF FIREWOOD FALLS TO THE GROUND**

61. **SFX:** **MALEMBA RUNNING TOWARDS HER SON**

62. **MALEMBA:** **(yelling)** Chumba! Nashukuru u mzima!

63. **CHUMBA:** **(starts to scream)** joto… joto… Mama… joto…

64. **MALEMBA:** **(begins to cry)** Najua, Chumba, ni sawa sasa. Mama amerudi… Mama yuko nyumbani. Najua mwanangu… Itakuwa sawa. Mama yuko nyumbani na hatakuacha tena.

**HITIMISHO:**

Kwa bahati, Chumba alikuwa katika kijumba chake kidogo kando na kile cha mamake Malemba wakati moto ulipowashwa, na alijitoa mapema kabla moto kuenea. Malemba akamkumbatia kikiki mwanae Chumba, huku machozi ya uchungu yakimtiririrka njia mbili. Amerudi nyumbani, ijap nyumba yake imeteketea. Nyumba yake iliyokuwa gae sasa imekuwa jivu. Lakini kwa sasa, hajali: mikononi mwake amemkumbatia mwanae wa pekee: kijana wake Chumba. Malemba amejikuza na maadili mazuri inapokuja kumhudumia mwanae Chumba. Hilo linatufikisha tamati ya kipindi hiki cha nne. Kutatokea nini kwa Malemba na Chumba hivi sasa? Je, Valerie atapata msaada wowote kule njiani? Na kivipi Kapaka ataishi na hali yake ile baada ya kumpeleka mkewe kujifungua mtoto? Kwa hayo na zaidi usibanduke wakati wa kipindi kijacho. Ikiwa unataka kusikiliza tena kipindi hiki au kipindi KIngine kijacho, tafadhali tembelea tovuti zetu za dw.de/lbe na utufahamishe yale wananchi wa taifa lenu wanayowatendea watu walio na maradhi ya akili. Mpaka wakati mwingine, kwaheri.